

Maswali

1. Paulo alienda mji gani kuhubiri Injili?
2. Jina la mungu mke mwenye watu waliabudu alikuwa anaitwa nani?
3. Wafua fedha waliuza nini?
4. Paulo alikaa akihubiri Efeso kwa muda gani?
5. Wakristo walifanya nini na vitabu vyao vya uchawi?
6. Mbona wafua fedha walikuwa na uoga?
7. Nani alipanga mkutano wa wafua fedha?
8. Wafua fedha na watu wote walienda wapi?
9. Watu wote walipiga kelele kwa masaa mawili wakisema nini?
10. Nani alifanya umati ukanyamaza?

Majibu

1. Paulo alienda Efeso kuhubiri Injili.
2. Mungu wa kike aliitwa Daina.
3. Vihekalu vya fedha na sanamu ya Daina.
4. Paulo alihubiri huko Efeso kwa miaka miwili.
5. Wakristo waliwasha moto mkubwa na wakachoma vitabu vyao vya uchawi.
6. Wakristo hawakuamini Daina mungu mke. Hawakununua vihekalu. Wafua fedha walikuwa na uoga kwa sababu watapoteza biashara zao.
7. Demetrio alipanga kuwe na mkutano wa wafua fedha.
8. Wafua fedha na watu wote walienda kwa jumba la michezo.
9. Kwa masaa mawili walipiga kelele wakisema, “Daina wa Efeso ni mkuu!”
10. Karani wa mji alinyamazisha watu na kuwambia waende nyumbani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



99 Ghasia kwa jumba la michezo

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume 19:23—41

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba sanamu zenye watu waliabudu hawakuwa mungu wa kweli. Mungu ni Mungu wapekee. Mungu husaidia wanaomwamini

Somo

Paulo alienda Efeso kuhubiri Injili. Paulo alifurahi kukutana na marafiki zake Akila na Prisila huko Efeso. Walimsaidia kuhubiri Injili kule.


Efeso ulikuwa mmoja ya miji ya Asia. Watu wa Efeso waliabudu mungu mke aliyeitwa Daina (wakati mwingine aliitwa Artemi). Watu wa Efeso walijenga hekalu nzuri ya Daina. Watalii wengi walikuja Efeso kuabudu mungu mke Daina. Wachawi walileta vitabu vyao vya uchawi na hirizi. Hizi zilitakiwa kuleta bahati nzuri na kuwalinda kutoka kwa hatari yeyote.

Mfua fedha aliua vihekalu na mifano ya fedha ya muundo wa Daina. Wachawi na wafua fedha walitajirika sana kwa kuuza hivi vitu kwa watalii.


Mfano wa mungu mke Daina



Kwa karibu mwaka mmoja Paulo alihubiri Efeso. Watu wengi waliamini na wakabatizwa. Watu walipokuwa Wakristo hawakuamini kwa sanamu wala miungu ya uongo tena. Hawakuamini kwa uchawi. Hawakuabudu Daina mungu mke tena. Hawakununua hirizi za uchawi na vihekalu vya Daina. Siku moja Wakristo walileta vitabu vyenye walikuwa wameviamini. Walilundika hivyo vitabu pamoja na kuvichoma. Umati wa watu ulikuja kuangalia moto mkubwa wenye ulikuwa unachoma vitabu vya uchawi.



Wafua fedha walikuwa na wasiwasi juu ya biashara yao. Kulikuwa na watu wengi waliosikiliza Paulo na wakaamini kwa Mungu. Paulo alikuwa akihubiri kwamba mungu mke Daina alikuwa ni mungu wa



uongo. Wakristo hawakuamini Daina. Wafua fedha walikundua kwamba h a w a k u k u w a wakiuza vihekalu vya fedha vya Daina vile walikuwa wakiuza. Hawakuwa wakipata pesa nyingi.

Sanamu ya
Daina
pekee 50

Demetrio alikuwa ndiye mkuu wa wafua fedha. Demetrio alipanga wawe na mkutano. Alizungumza na wafua fedha wote, akasema, “Tuna biashara mzuri sana hapa Efeso. Tunatengeneza pesa nyingi sana kutoka kwa mauzo ya vihekalu vya Daina. Paulo ako anafundisha kwamba sanamu za fedha na dhahabu si mungu kamili. Watu wengi wako wanaamini Paulo. Watu wengi wamekuwa Wakristo. Kuna hatari kwamba tutapoteza biashara yetu. Watu watakataa kukuja Efeso kuabudu mungu mke Daina.”

Wafua fedha walikasirika sana. Walikimbia kwa barabara za Efeso zote wakipiga makelele. Wakisema, “Daina wa efeso ni mkuu! Daina wa Efeso ni mkuu!” Bunde tu, mji wa Efeso ulijaa ghasia. Watu wote walikimbia kwa jumba la michezo. Waliburura marafiki wawili wa Paulo. Paulo alishawishiwa kwamba asiende kwa jumba la michezo. Watu wangemuua.

Jumba la michezo lilijaa watu. Kila mtu alikuwa anapiga kelele ya juu sana. Wengine walikuwa wakisema hivi na wengine wakisema tofauti na wale. Wengi wa huo umati hawakuelewa nini ilikuwa ikiendelea. Rafiki wa Paulo alienda mbele ya umati ili azungumze. Waliacha kupiga kelele ili wamsikilize. Lakini watu walipokundua kwamba yeye ni Myahudi, walianza kupiga kelele tena. Walipiga kelele kwa masaa mawili. Wakisema, “Daina wa Efeso ni mkuu! Daina wa Efeso ni mkuu!”

Baadaye karani wa mji aliwanyamazisha. Aliwambia, “Enyi wanaume wa Efeso, kila mtu anajua kwamba mji wa efeso ni mtunzaji wa Daina mungu mke. Inabidi mnyamaze na muaje kufanya ghasia. Kama Demetrio na wafua fedha wanamalalamishi juu ya mtu yeyote, lazima waende kotini. Watawala wa Kirumi wakisikia haya yote tutaadhibiwa.” Alipomaliza aliambia kila mtu aende nyumbani. Baadaye Paulo aliondoka Efeso.